 - Benki Kuu ya Tanzania na Serikali kwa usimamizi mzuri wa sekta ya huduma za fedha.
 - Washirika na watoa huduma mbalimbali.

5.2 Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji

Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa yake kama ifuatavyo:

Mkakati wa biashara

- 5.2.1 Mwaka wa fedha 2021 ulikuwa wa nne katika miaka mitano ya mkakati wa biashara wa muda wa katika, ambapo Benki ilidhamiria kushughulikia mapungufu ya utendaji na kuongeza ubora wa biashara ili kuendeleza ukuaji.
- 5.2.2 Faida ya kampuni tanzu ya Bima (*CRDB Insurance Broker Ltd*) ilipungua kutokana na mageuzi na mabadiliko ya kanuni za Benki Kuu ambayo ilisitisha huduma za udalali wa bima kwa mabenki ili kutoa fursa kwa mabenki kutoa huduma za bima bila kupitia kwa madalali. Benki imetekeleza takwa hilo kwa kuunganisha kikamilifu shughuli za bima na huduma kwa wateja wadogo na katika, na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma za bima.
- 5.2.3 Benki ilitekeleza mkakati maalum wa kupata wateja wapya kupitia mauzo yenye kulenga mnyororo wa thamani na kutanua wigo wa njia mbadala za kutoa huduma kwa kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara.
- 5.2.4 Benki iliboresha bidhaa zake kuu kuendana na mahitaji maalum ya wateja wake na hivyo kusababisha kuongezeka kwa matumizi ya huduma na bidhaa.
- 5.2.5 Benki ilishuhudia kuimarika kwa biashara kutoka kwa wateja wakubwa ambao walikuwa wameathiriwa na changamoto zilizojitokeza ulimwenguni. Benki ilinufaika kutokana na kubatilishwa kwa vizuizi vya kuvuka mipaka na washirika wake wa kibashara kama vile Kenya, Uganda na Rwanda kutokana na suala la UVIKO-19. Makubaliano katika ya nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuhusu mbinu za pamoja kukabiliana na janga la UVIKO-19 yalikua na mchango mkubwa katika kufungua eneo la ukanda kibashara.
- 5.2.6 Uamuzi wa serikali ya Tanzania kuimarisha uhusiano na Kenya ulitoa msukumo uliohitajika kuimarisha biashara katika ya nchi hizo mbili. Kutokana na hilo, wateja wengi hasa walio kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo, walifaidika kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za kilimo kama vile nafaka na mazao ya bustani upande wa Kenya. Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu zilikuwa tayari kutoa bidhaa muhimu za kifedha na uwezeshaji ambao ulisaidia kuweka sawa mzani wa biashara kwa faida ya Tanzania.
- 5.2.7 Shilingi ya Tanzania ilikuwa imara kwa kipindi cha mwaka mzima, na kudumisha utendaji mzuri dhidi ya dola ya Marekani. Hii ilichangwa zaidi na upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na kurejea kwa shughuli za utalii, mauzo ya nje na fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.
- 5.2.8 Bima ya matibabu ilianzishwa kupitia vyama vya ushirika ili kuwahudumia wakulima wa sekta ndogo za kahawa, maziwa, tumbaku, mkonge, miwa, korosho na pamba. Ruzuku ya dola milioni 100 kutoka Mfuko wa Hali ya Hewa ya Kijani (*Green Climate Fund - GCF*) ambayo illidhinishwa hivi karibuni itaimarisha zaidi uwezo wa Benki kuwekeza kwenye sekta ya kilimo.

Maboresho ya Mfumo wa Kidijitali

- 5.2.9 Benki ilifanya uwekezaji mkubwa katika kuimarisha uwezo wake wa TEHAMA na iliboresha matumizi kwenye mifumo yote ya kidijitali ikiwa ni pamoja na wavuti (benki kwa njia ya mtandao), ATM na mashine za malipo. Benki ilibadilisha zaidi ya ATM 100, kuanzisha kikokotoo cha Mkopo wa E-Loan kwa watumiaji wa wavuti, kuboresha usajili wa manunuzi mtandaoni, na kuboresha wigo wa bidhaa za kielektroniki, kurahisisha miamala ya ndani ya Tanzania yaani (*Tanzania Inter-Bank Settlement System - TISS*).

Ushirikiano na Wadau

- 5.2.10 Benki iliendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenyе lengo la kudumisha mahusiano na wateja ikiwemo kuanzisha ubia baina yake na Shirika la Posta Tanzania (Tanzania Posts Corporation-TPC) kwa ajili ya kutoa huduma za kibenki kupitia vituo 90 vya huduma viliyyosambaa nchi nzima. Ubia huo unaruhusu wateja wanaotafuta huduma za benki kuzipata katika vituo vya TPC, pamoja na mtandao wa wakala zaidi ya 19,000 na zaidi ya matawi 250.
- 5.2.11 Benki iliyafikia makundi tofauti ya wadau na kuwahuishaa kwa namna mbalimbali kuhusu masuala muhimu yenyе uhusiano wa moja kwa moja kwenye biashara. Moja ya tukio muhimu ilikua ni ziara ya Mheshimiwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bi. Samia Suluhu Hassan kwa kampuni tanzu ya Burundi, iliyopo mjini Bujumbura, Burundi wakati wa ziara yake ya kwanza ya kiserikali nchini humo mwezi Julai, 2021. Ushirikiano mwininge muhimu ni ushiriki katika Kongamano la Hali ya Hewa la Umoja wa Mataifa lilofanyika jijini Glasgow, Scotland ikiwa ni sehemu ya juhudhi zinazoendelea kwa Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu kushiriki katika masuala endelevu ya utunzaji wa mazingira.

Uwekezaji kwenye Raslimali Watu

- 5.2.12 Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu ziliwekeza katika rasilimali watu kwa kuvutia na kuhakikisha wafanyakazi yenyе vipaji wanaendelezwa. Mafunzo maalum ikiwemo kuanzisha kambi za masuala ya ustawi wa afya ya wafanyakazi na kuandaa mashindano kati ya idara na kanda yalitolewa kwa ajili ya kukuza mahusiano ya wafanyakazi na kuboresha ustawi wao wa kimwili na kiakili. Programu ya kujifunza kwa njia ya mtandao inayotambulika kimataifa-*UDEMY* ilianzishwa kukuza ari ya wafanyakazi kujifunza na kuboresha uwezo wao kiutendaji.
- 5.2.13 Mkurugenzi Mtendaji aliwashukuru wafuatao:
- (i) Wanahisa wote wa benki kwa kuendelea kuwekeza ndani ya Benki.
 - (ii) Bodi ya Wakurugenzi kwa mchango wake thabiti, na hasa katika uongozi na weledi ambao umeongoza Benki kupata matokeo mazuri.
 - (iii) Wafanyakazi kwa ustahimilivu katika kukabiliana na changamoto mbalimbali.
 - (iv) Washirika wa utoaji huduma kama vile mawakala wa CRDB, watoa huduma na wazabuni.
 - (v) Wateja kwa kuipa Benki fursa adhimu ya kuwashudumia.
 - (vi) Wadau wa nje akiwemo mdhibiti wa sekta, Benki Kuu ya Tanzania, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika masoko ambako Benki inafanya biashara.

5.3 Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2021

Afisa Mkuu wa Fedha Bw. Frederick Bayona Nshekanabo aliwasilisha Taarifa ya Hesabu za Benki zilizokaguliwa kwa mwaka 2021 kama ifuatavyo:

Matokeo ya Kifedha

- 5.3.1 Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu zilifanya vyema katika kutekeleza mkakati wa muda wa kati na katika kufikia malengo ya mwaka ya kiutendaji. Benki ilipitia na kurekebisha viwango vyake vya udhibiti wa hatari ili kuakisi mabadiliko mapana ya kiuchumi na kuweka mkazo wa makundi ya wateja yenyе changamoto zaidi.
- 5.3.2 Faida baada ya kodi iliongezeka kwa asilimia 62.3 kutoka shilingi bilioni 165.2 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 268.2. Hii ndiyo faida kubwa zaidi iliyowahi kuripotiwa katika historia ya Benki na inatoa taswira ya thamani ya mageuzi endelevu ambayo benki imefanya katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.
- 5.3.3 Jumla ya mapato ya uendeshaji kabla ya gharama za tengo la mikopo chechefu yaliongezeka kwa asilimia 14.3 kutoka shilingi bilioni 808.7 hadi shilingi bilioni 924.0 mwaka 2020. Ukuaji huo ultokana na ongezeko la asilimia 11.3 la mapato halisi ya riba, iliyotokana na ukuaji mzuri wa mikopo ya reja reja na malipo ya awali.

- 5.3.4 Uwekezaji wa Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu katika teknolojia, hasa katika uimarishaji wa huduma ulizaa matunda kwa ukuaji unoonekana katika mapato yasiyofadhiliwa kutokana na ada na kamisheni. Kufikia mwisho wa mwaka, mapato yasiyo ya riba yalikua kwa asilimia 24.4, yakichochewa na ada zinazohusiana na mikopo na mapato ya miamala kutoka kwa huduma ya *SimBanking*. Miamala ya *SimBanking* iliongezeka kwa kuwa wateja waliendelea kuchagua kutumia njia mbadala kufanya miamala. Huduma ya *SimBanking* ilipata mvuto zaidi kwa watumiaji katika mwaka huo kufuatia uboreshaji uliofanywa.
- 5.3.5 Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu ziliharakisha utekelezaji wa mipango ya kimkakati ili kupata uwiano mzuri wa gharama. Kipaumbele kilikuwa kuongeza tija na kupunguza gharama za uendeshaji. Gharama za uendeshaji ziliongezeka kwa asilimia 3 kutoka shilingi bilioni 499.5 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 513.3. Uwiano wa ufanisi uliimari kwa kiasi kikubwa hadi kufikia asilimia 55.3 kutoka asilimia 61.6 mwaka 2020. Uwiano huu ulifikiwa kutokana na agizo la Benki Kuu ya Tanzania lililotolewa katika robo ya kwanza ya 2021, lilitozitaka benki kuwa na uwiano wa gharama na mapato usiozidi asilimia 55 hadi ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022.
- 5.3.6 Mizania ya Benki ya CRDB ilikua kwa asilimia 23 kutoka shilingi trilioni 7.2 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 8.8 mwaka 2021. Ukuaji huo ultokana na ukuaji wa amana za wateja kwa asilimia 19.4 na ukuaji wa fedha za wanahisa kwa asilimia 20.6. Matokeo hayo yalisabishwa na ukuaji wa mikopo kwa wateja wakubwa na mikopo ya nyumba (*mortgage loans*). Mikopo ya wateja wakubwa ilikua kwa asilimia 49 kutoka shilingi trilioni 1.5 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 2.2 mwaka 2021 ikiashiria kuendelea kuimari kwa uchumi.
- 5.3.7 Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu ziliendelea kudumisha hali nzuri ya ukwasi kwa uwiano wa asilimia 27.5 juu ya uwiano unaotakiwa na mdhibiti wa sekta wa asilimia 20; uwiano wa mkopo kwa amana ulisalia kuwa asilimia 78.8. Kimkakati, Benki iliendelea kuboresha mchanganyiko wa upatikanaji wa amana za bei nafuu na zenye kukaa muda mrefu. Kutokana na hali hiyo, amana za wateja zilikua kwa asilimia 19.4 kutoka shilingi trilioni 5.4 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 6.5 mwaka 2021.
- 5.3.8 Benki iliendelea kutekeleza mipango ya kimkakati yenyе lengo la kudumisha ubora wa mikopo, ikijumuisha kutoa mikopo katika sekta tofauti, kupunguza viashiria vya hatari vya mikopo na upatikanaji wa dhamana za muda mrefu kuitia washirika wa kimkakati. Mafanikio yalipatikana kuitia mkakati thabiti wa kuzuia mikopo chechefu kwa kuboresha usimamizi wa marejesho ya mikopo.
- 5.3.9 Uchanganuzi wa kanzidata na matumizi ya Mfumo wa Tahadhari ya Mapema ulianzishwa kubashiri mapema mikopo isiyolipika. Mfumo huo ulienda sambamba na ufuutiliaji wa karibu wa marejesho. Matumizi ya teknolojia yalichangia kwa kiwango kikubwa kuimari kwa uwezo wa kuhudumia wateja kuitia mfumo wa kidijitali (e-Collect).

Utendaji wa Kampuni Tanzu

- 5.3.10 Kampuni tanzu ziliendelea kupata matokeo chanya ya utendaji. Kampuni tanzu ya Burundi ilipata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 12.8, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 15.3 kutoka shilingi bilioni 11.1 mwaka 2020. Mali za kampuni tanzu zilikua kwa asilimia 57.0 hadi shilingi bilioni 551.1. Jumla ya amana zilikua kwa asilimia 65.8 hadi shilingi bilioni 329.4. Kampuni tanzu ya bima iliripoti kushuka kwa faida baada ya kodi kwa asilimia 76.8 hadi shilingi bilioni 0.8 kutokana na kuhamishwa kwa biashara ya udalali wa bima kwenda kampuni mama, jambo lilitosababishwa na uimarishaji wa biashara ya bima kuitia kwa kampuni mama.
- 5.3.11 Benki ilifunga mwaka kwa uwiano wa mikopo chechefu wa asilimia 3.3 dhidi ya kiwango cha mdhibiti wa sekta cha asilimia 5. Benki itaendelea kufuatilia kwa karibu mikopo, haswa kwa wateja ambao bado wanaendelea kurejea katika hali ya kawaida baada ya matokeo hasi ya janga la UVIKO-19 ili kudumisha ubora wa mali, kuendelea kuzingatia usimamizi makini wa mtaji na kupunguza hatari kwa ujumla kuhakikisha matumizi bora ya mtaji.

5.4 Kujadili Taarifa za; Mwenyekiti wa Bodii, Mkurugenzi Mtendaji na Hesabu Zilizokaguliwa

Wanahisa **WALIPOKEA** Taarifa za; Mwenyekiti wa Bodii, Mkurugenzi Mtendaji na Hesabu Zilizokaguliwa na kuzijadili kama ifuatavyo:

- 5.4.1 **ILISHAURIWA** kwamba Benki ianzishe dawati la miradi ya kilimo.
- 5.4.2 **ILISHAURIWA** kwamba Mkutano Mkuu ufanyike sehemu nyingine tofauti na mkoa wa Arusha. Menejimenti ifikirie kuandaa Mkutano Mkuu Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma.
- 5.4.3 **ILISHAURIWA** kwamba Menejimenti ifikirie uwezekano wa kupunguza kiwango cha riba kwa mikopo inayotolewa kwa Wanahisa.
- 5.4.4 **ILISHAURIWA** kwamba Benki itoe elimu zaidi kwa wakulima ili waweze kuchangamkia fursa za mikopo zinazotolewa na Benki ili kukuza kilimo. Benki iwe makini na ukuaji wa mizania hasa upande wa mikopo. **ILIELEZWA** kwamba Benki itaendelea kutoa elimu kwa wakulima na kuwa makini katika ukuaji wa mizania na itajielekeza katika kukuza mtaji.
- 5.4.5 **ILIUULIZWA** iwapo Benki inatoa mikopo kwenye kilimo cha umwagiliaji au kilimo cha msimu kutegemea mvua. **ILIELEZWA** kwamba Benki ina utaratibu mzuri wa kutoa mikopo kwenye sekta ya kilimo na riba inayotolewa ni nafuu. Benki inatarajia kilimo kuwa cha kisasa nchini na itaendelea kupanua wigo wa maeneo ya kilimo yatakayofaidika na mikopo.
- 5.4.6 **ILISHAURIWA** kwamba Benki iongeze kiwango inachotoa kwa shughuli za kijamii kutoka asilimia moja (1%) inayotolewa sasa kutoka kwenye faida ghafi ya Benki na kupanua shughuli zake za huduma kwa jamii nchi nzima. **ILIELEZWA** kwamba Benki itatathmini uwezekano wa kuongeza kiwango kama ilivyoshauriwa na kupanua shughuli za kijamii nchi nzima.
- 5.4.7 **ILISHAURIWA** kwamba Benki iandae dodoso ili kupata maoni ya wanahisa/wateja kuhusu huduma zitolewazo na Benki kuboresha utendaji. **ILIELEZWA** kwamba Benki itaendelea kufanya tafiti mbalimbali kujua mahitaji ya wateja.
- 5.4.8 **ILISHAURIWA** kwamba Benki itoe elimu ya uwekezaji kwa vijana.
- 5.4.9 **ILISHAURIWA** kwamba Benki ifanye jitihada ili kuimarishe bei ya hisa zake sokoni.
- 5.4.10 Benki **ILISHAURIWA** kuongeza mtaji kwenye benki ya TACOBA kuiwezesha benki hiyo kuijendesha na kupata faida. **ILIELEZWA** kwamba Benki ina mikakati ya kuhakikisha TACOBA inaendelea na jitihada za kuweza kuijendesha na kupata faida.
- 5.4.11 **PONGEZE** zilitolewa kwa Bodii ya Wakurugenzi, Afisa Mtendaji Mkuu na Menejimenti kwa jitihada za kupanua huduma nchi jirani kwa kuanzisha kampuni tanzu katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, ukuaji wa faida, kupungua kwa mikopo chechefu na kushiriki katika masuala ya utunzaji wa mazingira.

6.0 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA 2021

- 6.1 Bodii ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** gawio kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2021 liwe shilingi 36/= kwa kila hisa kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 22 Aprili 2022 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 13 Juni, 2022.
- 6.2 **ILIAZIMIWA** kuwa gawio kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2021 liwe shilingi 36/= kwa kila hisa kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 22 Aprili, 2022 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 13 Juni, 2022.

7.0 KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI

- 7.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** kwamba jumla ya ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa mwaka 2022 iwe shilingi 965,000,000/= ambazo zitatumika pia kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.
- 7.2 **ILIAZIMIWA** kwamba ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa Mwaka 2022 iwe shilingi 965,000,000 /= ambazo pia zitatumika kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.

8.0 KUTEUA WAKAGUZI WA NJE WA HESABU

- 8.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** kwamba Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu ya *Ernst and Young* ya Tanzania, S.L.P 2475, Dar es Salaam, iteuliwe kuwa Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake tanzu kwa mwaka 2022 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.
- 8.2 **ILIAZIMIWA** kwamba Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu ya *Ernst and Young* ya Tanzania, S.L.P 2475, Dar es Salaam, iteuliwe kuwa Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake tanzu kwa mwaka 2022 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

9.0 KUCHAGUA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

- 9.1 Katibu aliwaeleza wanahisa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Benki, Mkurugenzi wa Benki atahudumu kwenye Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuomba kuchaguliwa tena. Hivyo kila mwaka kuna wakurugenzi wa Bodi ambao wanastaafu kutoa nafasi kwa uchaguzi kufanyika. Mwaka 2022 Wakurugenzi watatu wa Bodi amba ni Bw. Abdul Ally Mohamed anaewakilisha kundi la wanahisa wenyе hisa chini ya asilimia moja (1%), Dkt. Fred Matola Msemwa anaewakilisha kundi la Wanahisa wenyе Hisa katи ya asilimia moja na kumi (1% - 10%) na Bw. Martin Steven Warioba ambae ni Mjumbe Huru wa Bodi wanatakiwa kustaafu baada ya kumaliza kipindi cha miaka mitatu. Wakurugenzi hao waliomba kuchaguliwa tena baada ya kustaafu.
- 9.2 Katibu aliwaeleza Wanahisa kwamba muda wa utumishi wa Wajumbe wawili wa Bodi ya Wakurugenzi Dkt. Ally Hussein Laay na Mhandisi Boniface Charles Muhegi ulikuwa umefikia ukomo kutokana na kanuni mpya ya Benki Kuu ya utawala bora ya mwaka 2021, kipengele namba 12 ambacho kinataka Mjumbe wa Bodi kuhudumu katika taasisi ya fedha kwa kipindi kisichozidi miaka 10 mfululizo. Kwa mujibu wa kanuni hiyo wajumbe hao wawili walikuwa wamefika ukomo wa muda wao wa ukurugenzi wa Bodi. Katibu aliwaeleza Wanahisa kwamba Benki Kuu imeongeza muda wa kuhudumu katika Bodi ya Wakurugenzi wa wajumbe hao wawili kwa kipindi cha miaka 3 kutoka mwaka 2022 hadi mwaka 2025 kuruhusu Benki kujandaa kutekeleza matakwa ya kanuni mpya za utawala bora.
- 9.3 Bodi ya Wakurugenzi walipendekeza Wajumbe hao wawili Dkt. Ally Hussein Laay na Mhandisi Boniface Charles Muhegi kupitishwa kuwa wajumbe wa Bodi kuwakilisha kundi la Wanahisa wenyе hisa chini ya asilimia moja (1) kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia Mei 2022 hadi Mei 2025.
- 9.4 Wagombea wa nafasi ya Mjumbe wa Bodi kutoka kundi la wanahisa wenyе hisa chini ya asilimia 1 walikuwa Bw. Abdul Ally Mohamed na Mh. Frederick Tluway Sumaye.
- 9.5 Mgombea nafasi ya Mjumbe wa Bodi kutoka kundi la wanahisa wenyе hisa katи ya asilimia 1 na 10 alikuwa Dkt. Fred Matola Msemwa.
- 9.6 Wagombea wa nafasi ya Mjumbe Huru wa Bodi walikuwa Bw. Martin Steven Warioba na Mhandisi Jameson James Kasati
- 9.7 Mwenyekiti aliwakaribisha wagombea wote kujieleza mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa dakika tatu (3) na kujibu maswali yatakayoulizwa.

- 9.8 Katibu alitoa maelezo jinsi ya kupiga kura kidijitali na uchaguzi ulifanyika kama ilivyopangwa.
- 9.9 Matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi wanaowakilisha kundi la Wanahisa wenyе hisа chini ya asilimia 1: Kura zilipigwa kulingana na idadi ya hisa kundi hili zilizowakilishwa kwenye Mkutano Mkuu.**

Na.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Bw. Abdul Ally Mohamed	459,667,322	95
2.	Mh. Frederick Tluway Sumaye	26,247,421	5
Jumla		485,914,743	100

- 9.10 Mwenyekiti alimtangaza Bw. Abdul Ally Mohamed kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha kundi la wanahisa wenyе hisа chini ya asilimia 1 baada ya kupata asilimia 95 ya kura zilizopigwa.
- 9.11 Mwenyekiti alimtangaza Mh. Frederick Tluway Sumaye kuwa kwenye orodha ya akiba. Mh. Sumaye alipata asilimia 5 ya kura zilizopigwa.
- 9.12 Bw. Abdul Ally Mohamed aliwashukuru wanahisa kwa kumchagua kwa kipindi kingine cha miaka mitatu (3) na kuwaahidi kuwa ataendelea kutekeleza majukumu yake akishirikiana na wajumbe wengine wa Bodi katika kutoa miongozo itakayosaidia Benki kuwa na mafanikio zaidi.
- 9.13 Matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi wanaowakilisha kundi la Wanahisa wenyе hisа katи ya asilimia 1 na 10: Kura zilipigwa kulingana na idadi ya hisa kundi hili zilizowakilishwa kwenye Mkutano Mkuu.**

Na.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Dkt. Fred Matola Msemwa	376,503,131	100
Jumla		376,503,131	100

- 9.14 Mwenyekiti alimtangaza Dkt. Fred Matola Msemwa kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha kundi la wanahisa wenyе hisа katи ya asilimia 1 na 10 baada ya kupata asilimia 100 ya kura zilizopigwa.
- 9.15 Dkt. Fred Matola Msemwa aliwashukuru wanahisa kwa kumchagua na kuahidi kutumia taaluma na uzoefu wake kwa kushirikiana na wajumbe wengine wa Bodi kuleta matokeo chanya.
- 9.16 Matokeo ya uchaguzi wa Mjumbe Huru wa Bodi. Kura zilipigwa kulingana na idadi ya hisa kundi hili zilizowakilishwa kwenye Mkutano Mkuu.**

Na.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Bw. Martin Steven Warioba	1,118,331,171	60
2.	Mhandisi Jameson James Kasati	751,281,412	40
Jumla		1,869,612,583	100

- 9.17 Mwenyekiti alimtangaza Bw. Martin Steven Warioba kuwa Mjumbe Huru wa Bodi baada ya kupata asilimia 60 ya kura zilizopigwa.
- 9.18 Bw. Warioba aliwashukuru wanahisa kwa kumchagua kwa kipindi kingine kuwa Mjumbe wa Bodi na kuwaahidi kufanya kazi kwa bidii zaidi kwa maendeleo ya Benki.
- 9.19 Mwenyekiti alimtangaza Mhandisi Kasati kuwa kwenye orodha ya akiba. Mhandisi Kasati alipata asilimia 40 ya kura zilizopigwa.

10.0 KUJADILI MAPENDEKEZO KUTOKA KWA WANAHISA

Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu alitangaza kuwa hakuna mapendekezo yaliyopokelewa kutoka kwa wanahisa.

11.0 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Hayakuwepo mengineyo kutoka kwa Wanahisa.

12.0 KUPANGA MAHALI NA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NANE

- 12.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane (28) wa Benki ya CRDB Plc ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 20 Mei, 2023 Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi.
- 12.1 **ILIAZIMIWA** kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane (28) wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 20 Mei, 2023 Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi.

13.0 KUFUNGA MKUTANO

- 13.1 Mwenyekiti wa Bodi aliwashukuru wanahisa na wadau kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu na kuahidi kuwa maoni na masuala yote yaliyowasilishwa na wanahisa yatafanyiwa kazi na Menejimenti.
- 13.2 Alimpungeza Balozi wa Denmark nchini Tanzania Bi Mette Nørgaard Dissing-Spandet kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu na kutoa mawazo yenye tija kwa maendeleo ya Benki.
- 13.3 Alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Benki ya CRDB Dkt. Charles Kimei (MB) kwa mchango wa mawazo.
- 13.4 Alitoa pongezi kwa Benki Kuu ya Tanzania, CMSA na DSE kwa usimamizi na kutoa miongozo kwa maendeleo ya sekta ya Benki na masoko ya mitaji.
- 13.5 Aliwashukuru wajumbe wa Bodi na kuwakaribisha wajumbe wapya wa Bodi waliochaguliwa. Aliwapongeza wagombea wa nafasi za ujumbe wa Bodi ambao kura hazikutosha.
- 13.6 Alipongeza Bodi za Wakurugenzi za Benki ya CRDB Burundi S.A., CRDB Insurance Broker Ltd, Tandahimba Community Bank Plc (TACOBA) na Kilimanjaro Community Bank Limited (KCBL) kwa kazi nzuri.
- 13.7 Aliwapongeza wafanyakazi wa Benki ya CRDB kwa mafanikio yaliyopatikana na kuwataka kuendelea kujituma ili kupata mafanikio makubwa zaidi.
- 13.8 Alipongeza sekretarieti kwa maandalizi mazuri ya Mkutano Mkuu na Semina.
- 13.9 Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 9:00 alasiri.

IMETHIBITISHWA

MWENYEKITI

KATIBU

TAREHE

**Dondoo Na. 4 YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA SABA WA WANAHISA WA CRDB BANK PLC
ULIOFANYIKA JIJINI ARUSHA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA ARUSHA (AICC),
UKUMBI WA SIMBA TAREHE 21 MEI 2022**

NO	KUMB.	MAPENDEKEZO/USHAURI	UTEKELEZAJI
1.0	7.0	KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA 2020	
1.1	7.2	ILIAZIMIWA kuwa Gawio kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 liwe shilingi 36/= kwa kila hisa kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 22 Aprili, 2022 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 13 Juni, 2022.	Gawio la shilingi 36/= kwa hisa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 lilipwa kuanzia tarehe 13 Juni, 2022.
2.0	8.0	KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI	
2.1	8.3	ILIAZIMIWA kuwa ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka 2022 iwe shilingi 965,000,000 /= ambazo pia zitatumika kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi ya Wakurugenzi zilizopo sasa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.	Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka 2022 ni shilingi 965,000,000 /= ambazo pia zitatumika kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi ya Wakurugenzi zilizopo sasa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.
3.0	9.0	KUTEUA WAKAGUZI WA NJE WA HESABU	
3.1	9.3	ILIAZIMIWA kwamba Kampuni ya Ugazi wa Hesabu ya Ernst and Young Tanzania ya S.L.P 2475, Dar es Salaam, ndio Wakagazi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake Tanzu kwa mwaka 2022 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.	Kampuni ya Ugazi wa Hesabu ya Ernst and Young Tanzania ya S.L.P 2475, Dar es Salaam, ndio Wakagazi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake Tanzu kwa mwaka 2022 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.
4.0	10.0	KUCHAGUA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI	
4.1	10.8	Mwenyekiti alimtangaza Bw. Abdul Mohamed kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha Kundu la Wanahisa wenye hisa chini ya asilimia 1 baada ya kupata kura nyingi kuliko wagombea wengine.	Wajumbe wote wa Bodi waliochaguliwa wameidhinishwa na Benki Kuu.
	11.12	Mwenyekiti alimtangaza Dkt. Fred Msemwa kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia 1 na 10.	
	11.15	Mwenyekiti alimtangaza Bw. Martin Warioba kuwa Mjumbe Huru wa Bodi.	

NO	KUMB.	MAPENDEKEZO/USHAURI	UTEKELEZAJI
5.0	13.0 KUPANGA MAHALI NA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NANE		
5.1	13.2	ILIAZIMIWA kwamba Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 20 Mei 2023 jijini Dar es salaam kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi.	Ili kuendana na mkakati mpya wa Benki wa 2023 – 2027, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane wa Wanahisa wa Benki ya CRDB utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 20 Mei 2023 katika ukumbi wa Simba uliopo kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi na kuidhinishwa na Wanahisa wanaomiliki zaidi ya asilimia 50 ya hisa za Benki kwa mujibu wa katiba ya Benki na sheria ya makampuni namba 12 ya mwaka 2002.

Bw. Abdulmajid M. Nsekela

MKURUGENZI MTENDAJI

Dondoo Na. 5 TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MWAKA 2022

5.1 KUPOKEA TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI

(Taarifa itaambatishwa)

Wanahisa wanaombwa kupidisha azimio la kuipokea taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.

5.2 KUPOKEA TAARIFA YA HESABU

(Taarifa itaambatishwa)

Wanahisa wanaombwa kupidisha azimio la kuipokea taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2022.

5.3 GAWIO KWA MWAKA 2022

5.3.1 Pendekezo

Kwa mujibu wa sehemu ya VIII ya Katiba ya Kampuni, Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza gawio kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2022 liwe Shilingi 45/= kwa kila hisa kwa wanahisa watakaokuwepo kwenye daftari litakapofungwa tarehe 23 Mei 2023 na malipo yafanywe kuanzia tarehe 05 Juni 2023.

5.3.2 Kinachohitajika

Wanahisa wanaombwa kupidisha azimio la kuafiki pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kwamba gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2022 liwe shilingi 45/= kwa hisa kwa wanahisa watakaokuwepo kwenye daftari litakapofungwa tarehe 23 Mei 2023 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 05 Juni 2023.

Dondoo Na. 6 KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI

6.1 Pendekezo

Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza jumla ya ada kwa Wakurugenzi iwe shilingi 965,000,000/= kwa mwaka 2023 ambazo zitatumika pia kuwalipa wajumbe kwenye kamati nne za Bodi zilizopo hivi sasa.

6.2 Kinachohitajika

Wanahisa wanaombwa kupidisha azimio la kuafiki pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi na kupidisha jumla ya ada kwa Wakurugenzi ya Shilingi 965,000,000/= kwa mwaka 2023 ambazo zitatumika pia kuwalipa wajumbe kwenye kamati nne za Bodi zilizopo hivi sasa.

Dondoo Na. 7 KUTEUA WAKAGUZI WA HESABU

7.1 Mapendekezo

Bodi ya Wakurugenzi, inapendekeza Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu wa nje, Ernst & Young ya S.L.P 2475 Dar es Salaam, iteuliwe kuwa Wakaguzi wa hesabu za Benki kwa mwaka 2023, kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

7.2 Kinachohitajika

Wanahisa wanaombwa kuitisha azimio la kuteua Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu wa nje, Ernst & Young ya S.L.P 2475 Dar es Salaam, kuwa wakaguzi wa Benki kwa mwaka 2023, kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Dondoo Na. 8 KUCHAGUA WAJUMBE WA BODI

- 8.1 Kwa mujibu wa Ibara ya 98 ya Katiba ya Benki, Mjumbe wa Bodi anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kisichozidi awamu tatu za miaka mitatu kila moja

8.2 Mgawanyo wa Umiliki wa Hisa hadi tarehe 01 Machi, 2022

No.	Makundi ya Umiliki wa Hisa	Asilimia	Idadi ya Hisa	Idadi ya wajumbe wa Bodi
1	Asilimia kumi na zaidi	34.3	894,828,676	3
2	Asilimia Moja hadi chini ya Asilimia kumi	25.0	651,813,909	2
3	Chini ya Asilimia Moja	40.7	1,065,195,999	4
4	Huru	0	0	3
	Jumla	100.0	2,611,838,584	

8.3 Wajumbe wa Bodi Wanaostaifu

Wajumbe wawili huru wa Bodi Watastaifu mwaka huu kama ifuatavyo:

- a) Prof. Neema Munisi Mori
- b) Bi Miranda Naiman Mpogolo

8.4 Nafasi za ujumbe wa Bodi

Kutokana na muongozo wa Benki Kuu, Wanahisa wanatakiwa kupiga kura kuchagua wajumbe wawili Huru wa Bodi.

8.5 Taratibu za kupiga kura

- a) Wanahisa wote watapiga kura kuwachagua wajumbe wawili huru wa Bodi.
- b) Wagombea watakaopata kura nyingi watatangazwa kuwa wajumbe wa Bodi. Wagombea wanaofuatia kwa idadi ya kura watawekwa kwenye orodha ya akiba ili kuchukua nafasi ya wagombea walioshinda uchaguzi iwapo hawataidhinishwa na Benki Kuu au kushindwa kuwa wajumbe wa Bodi kwa sababu nyingine yoyote.
- c) Kila mgombea atapewa dakika tatu (3) kujitambulisha na kujibu maswali atakayoulizwa na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu.
- d) Kura itapigwa kwa siri na itawakilisha idadi ya hisa.
- e) Majina ya wagombea walioshinda uchaguzi yatatangazwa na Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu.

8.6 Majina ya wagombea

Majina ya wajumbe Huru wa Bodi

- i) Prof. Neema M. Mori
- ii) Bi Miranda N. Mpogolo
- iii) Mhandisi Boniface Gissima Nyamo - Hanga
- iv) Bi Joyce Nkini Lwisi

8.7 Provisions of Law Related to the Election and Responsibilities of Directors.

a) Article 96 of CRDB Bank MEMARTS

"Each of the directors appointed or elected shall be a person with knowledge and experience required by law as well as in line with the skills gap which the Governance, Nomination and HR Committee shall have identified to be filled by the directors sought in the Nomination process.

Regulation 5 (2) (a) of the Banking and Financial Institutions Act (B&FI Act)

Provides that a Board Member shall have requisite experience in banking, finance, accounting, auditing, law or economics.

Article 112 of CRDB Bank MEMARTS

Provides that the office of director shall be vacated if the director:

112.1 ceases to be a director by virtue of any provision of the Act or he becomes prohibited by law for being a director or becomes elected as member of parliament; or becomes an office bearing politician, or

112.2 Pursuant to the provision of the Act and B&FI Act, be disqualified or ceases to hold office or prohibited from acting as such; or

112.3 becomes bankrupt or makes any arrangement or composition with his creditors generally; or

112.4 becomes of unsound mind; or

112.5 resigns his office by notice in writing to the bank; or

112.6 is removed from office pursuant to section 193 of Act; or

112.7 **is seventy or more years of age** (this has been removed from law) or is under 21 years of age; or

112.8 shall for more than six consecutive months have been absent without permission of the directors from meetings of the directors held during that period and the directors resolve that his office be vacated.

b) Regulation 19 of Licensing Regulations of BOT and Article 94 of CRDB Bank Articles provides that Member of the board shall be appointed subject to approval by the Bank of Tanzania

c) Section 7 Part II of Banking and Financial Institution Act 2006, No. 12 of 1991 Regulations - Character and Experience of Proposed members of the Board and Management Team provides that:

- (1) The Bank shall make an assessment as to whether the proposed members of the board of directors and senior management of a proposed institution are fit and proper persons. The quality and capability of board members and management shall be the most essential ingredient for a successful banking operation. Accordingly, applications for a banking licence shall undergo close scrutiny as to the character and experience of their proposed management and board members. The aforesaid assessment shall be conducted in accordance with the criteria set out in the First Schedule hereto.

The Bank shall evaluate and determine to the extent possible, that the proposed members of the board of directors and senior management team has the experience and ability to manage fund, credit evaluation, collection procedures, proper accounting systems, effective internal control, audit programmes and management of information systems.

As such, the bank will review the curriculum vitae or personal information/history of the proposed board members and management team. The Bank reserves the right to interview the proposed board members and the management team and may enquire as to past performance and reputation, skills including fund management, credit evaluation, collection procedures, proper accounting systems, effective internal control, capable internal audit programs, and effective management information systems.

- d) **Regulation 7 (3) of Banking Institution Act Internal Control and Internal Audit Regulations, 2014** stipulates that “the Audit Committee shall be composed of at least three non- executive directors. Two of whom shall be independent members (Shareholders owning less than 5% of Bank’s shares) having accounting, auditing, or related financial management experience”. Accordingly, the number of independent members must be minimum three pursuant to B & FIA requirements.

Dondoo Na. 9. MAPENDEKEZO KUTOKA KWA WANAHISA

❖ (Mapendekezo yataambatishwa).

Dondoo Na. 10. MENGINEYO

Kujadili mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.

Dondoo Na. 11 TAREHE YA MKUTANO UJAO

Pendekazo

Inapendekezwa kwamba Mkutano Mkuu wa ishirini na tisa ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 18 Mei 2024 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba.

Dondoo Na. 12 KUFUNGA MKUTANO





www.crdb.co.tz

